BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA WA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Nne – Tarehe 28 Novemba, 2016.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya 2005, Kuweka Masharti Bora zaidi kwa ajili ya Ufanisi na Usimamizi Imara wa Mfuko na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya 2005, Kuweka Masharti Bora zaidi kwa ajili ya Ufanisi na Usimamizi Imara wa Mfuko na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

137. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamepatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Jimbo na kwa kuwa baadhi yao wamejenga na wengine hawakujenga kabisa ofisi hizo mpaka leo.

Je, Serikali ni lini itawapa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi fedha za ujenzi wa Ofisi za Jimbo kwa yale majimbo ambayo hayana ofisi.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

134. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Katika mwezi wa Machi 2016 Serikali kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma iliunda chombo cha kitaifa cha majadiliano katika sekta ya Umma. Chombo hicho kimeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 80 cha Sheria No. 2 (2011) na Kanuni za Utumishi wa Umma 2014.

Je ni sababu gani zinazopelekea chombo hicho kutokufanya kazi tangu kuzinduliwa kwake Machi 2016.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

148. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwa kuwa majina ya Mikoa na Wilaya za Unguja hazitumii majina ya asili ya maeneo husika kama zilivyo Wilaya za Pemba (Mkoani, Chakechake, Wete na Micheweni).

Je, lini Serikali itabadilisha majina ya Mikoa yote na Wilaya za Unguja, kuwa katika majina yake ya asili.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

87. MHESHIMIWA ALI KHAMIS BAKARI (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Kwa kuwa suala la udhalilishaji limezidi hasa kwa watoto. Na kwa kuwa kumeonekana kuwepo kwa watoto kupewa ajira na kukosa kusoma kwa wakati katika maeneo ya masoko, bandarini, na katika fukwe kwa kupara samaki na usambazaji wa bidhaa.

(a) Je Serikali haioni watoto wale wanakosa haki yao ya msingi ya elimu.

(b) Ni lini Wizara itatoa elimu kwa jamii ili kutowakosesha watoto haki hiyo.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira :

48. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Tumeshuhudia kushuka kwa bei ya mafuta duniani na kuleta unafuu kwa watumiaji baada ya Tanzania Bara bei ya mafuta kushuka tofauti na Zanzibar na kusababisha kero hiyo ya bei kwa wananchi ambao walikuwa na matumaini makubwa ya kuona bei ya mafuta Zanzibar nayo inapungua.

(a) Je, ni sababu gani hasa za msingi mafuta yanapopanda bei katika soko la dunia na viwango vya soko la bei ya ndani hupanda bila ya bei kushuka yanapotokea mabadiliko ya unafuu katika soko la dunia.

(b) Kwa kuwa Serikali imeahidi maisha bora kwa wananchi wake, hatua ya kutopunguza bei wakati mafuta yameshuka bei katika soko la dunia ni kuwapunguzia ukali wa maisha au kuwaongezea ukali wa maisha wananchi hao.

(c) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Unguja na Pemba ambao nishati ya mafuta ndio tegemeo lao kubwa katika maisha yao ya kila siku yakiwemo mafuta ya taa.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

37. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imesema mpango wa kugawa VIHORI 500 uko pale pale kwa wakulima wa mwani kama utekelezaji wa kuendeleza zao hilo Zanzibar hayo yamesemwa na Waziri wa Kilimo tarehe 23/7/2016 hapo Pwani Mchangani.

a) Je, mpango huo unatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha muda gani baada ya wakulima kukabiliwa na mazingira magumu katika uvunaji wa zao hilo.

b) Je, Serikali imechukua hatua gani baada ya kuwepo kilio cha muda mrefu cha bei ndogo ya zao hilo wakati Serikali imekiri kuwa zao hilo ni la tatu katika mazao yanayochangia pato la Taifa baada ya kupatikana Bilioni 6.

c) Je, ni lini Serikali itaanza kununua zao hilo kama ilivyo kwa zao la karafuu ili wakulima wake wawe na soko la uhakika.

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko:

108. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Katika kipindi cha mwaka 2014 – 2015 Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya TZS Millioni 342.3 kwa wakulima 126 wa karafuu wa Unguja na Pemba.

(a) Je, kiasi gani mpaka sasa kilichorejeshwa.

(b) Je, kabla ya mkopo huu hakukuwa na wakulima wengine wanaodaiwa.

109. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Serikali hufanya vyanzo vya biashara ili kutoa huduma kwa wananchi wake au kupata mapato na manufaa ya watu wote, la kushangaza ni kwamba biashara hizo hufa au hufilisika na biashara hiyo hiyo anapopewa mfanyabiashara binafsi huimarika na kumnufaisha kwa kiasi kikubwa.

a) Je, kwa nini miradi ya biashara inayosimamiwa na Serikali huwa haifanyi vizuri zaidi ukilinganisha wakati anapopewa mtu binafsi.

b) Nini adhabu ya waliohusika kuleta hasara Serikali na kuikosesha mapato.

c) Serikali imejipanga vipi kurudisha biashara zake kama zamani ili kudhibiti biashara ambazo ni nguzo ya Serikali.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

13. MHESHIMIWA MOHAMMED SAID MOHAMMED (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Oman kupitia chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), ilianzisha kigoda cha Sultan Qabus Al -Busaid mwaka 2013.

a) Ni wanafunzi wangapi wamefaidika tangu kuanzishwa kwa programu hiyo.

b) Je, wanafunzi wangapi wamefaidika kwa mchanganuo wa ngazi ya Shahada ya Kwanza, Shahada ya Pili na Shahada ya Uzamivu (Phd).

c) Hadi kufikia Oktoba, 2016 ni kiasi gani cha fedha kimeshalipwa kwa kusomesha wanafunzi wote hao.

25. MHESHIMIWA DKT. MAKAME ALI USSI (Jimbo la Mtopepo) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Lengo kuu la mfumo wa Elimu kwa wote na kuweka utaratibu wa elimu bila ya malipo ni kuwapatia elimu muhimu wananchi wote ili kuwasaidia katika maisha yao.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwahamasisha na kuimarisha elimu ya watu wazima na vipi inawashirikisha katika masuala ya matamasha na maadhimisho mbali mbali ya elimu ili na wao wajione kuwa ni sehemu ya wanafunzi wanaoshirikishwa katika shughuli hizo.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuzisaidia familia maskini sana katika kuhakikisha kuwa na wao, hususan, watoto wao wanapatiwa elimu ili iwakomboe na janga hili la umasikini.

(c) Je, ni watu wazima wangapi wameendelezwa na Wizara hadi kufikia viwango vya Shahada ya Kwanza.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

63. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Ni kiasi gani cha fedha kimepangiwa katika ujenzi wa barabara ya Fuoni kwenda Tunguu.

Wizara ya Afya:

27. MHESHIMIWA NADIR ABDUL-LATIF YUSSUF (Jimbo la Chaani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa miongoni mwa malengo makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuimarisha huduma za afya katika maeneo ya vijijini. Hata hivyo, kukosekana kwa huduma ya afya katika kituo cha Chaani kulikosababishwa na uchakavu wa Kituo hicho kumepelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi waliokuwa wakikitegemea kituo hicho kwa ajili ya kupata huduma za afya.

(a) Ni lini Serikali itaanza kukamilisha ujenzi wa Kituo hicho.

(b) Ni hatua gani za dharura zitakazochukuliwa ili kuhakikisha wananchi wa Chaani wanapata huduma za afya huku wakisubiri kukamilika kwa ukarabati wa Kituo hicho cha afya.

30. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Moja ya mambo ambayo yanapewa kipaumbele na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuwapatia wananchi wake huduma nzuri za afya na katika kutimiza lengo hilo Serikali imekuwa ikijitahidi kujenga hospitali na vituo vya afya sehemu mbali mbali. Miongoni mwa hospitali hizo ni ya Mbuzini, Wilaya ya Magharibi A ambayo imepata bahati ya kutembelewa na Mhe. Dr. Ali Moh'd Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zaidi ya mara mbili na katika ziara zake hizo Mhe. Rais alitaka Wizara ya Afya kufanya haraka ili kumaliza ujenzi wa hospitali hiyo ili iwe hospitali ya Wilaya.

a) Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa hospitali hiyo katika kutekekelza agizo la Mhe. Rais na kuwapunguzia usumbufu wa ukosefu wa huduma bora wananchi wa Wilaya ya Magharibi A.

b) Ni lini ujenzi wa hospitali hiyo unatarajiwa kuanza tena.

c) Hivi sasa kuna mazungumzo yoyote baina ya Wizara yako na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, ambao ndio waanzilishi wa hospitali hiyo, katika kupanga mpango mkakati wa kumalizia ujenzi wa hospitali hiyo pamoja na uendeshaji wake.

III. HOJA ZA SERIKALI

Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya 2005, Kuweka Masharti Bora zaidi kwa ajili ya Ufanisi na Usimamizi Imara wa Mfuko na Mambo Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
28 Novemba, 2016.

(Amour M. Amour)
KNY. KATIBU WA BARAZA.